

AZIMIO

KWA KUWA, Shule za Umma za St. Louis ("SLPS") zina jukumu la kuhakikisha kuwa wanafunzi wote walio katika eneo zake wana uhuru wa kupewa elimu ya umma bila malipo kwa mujibu wa uamzi wa Mahakama Kuu ya Marekani katika Plyler v. Doe; na

KWA KUWA, Baraza kuu la Elimu linafahamu kwamba kukataliwa kuandikwa shuleni au kushiki mpango wowote wa wilaya kwa msingi wa kuwa mwanafunzi hawana vitambulisho ni ukiukaji wa Marekebisho ya Kumi na nne ya Katiba ya Marekani, na

KWA KUWA, Baraza kuu la Elimu linafahamu kwamba rekodi za wanafunzi wasio na vitambulisho zitalindwa chini ya Sheria ya Haki ya Familia ya kuwa na Faragha Kielimu (FERPA) na kuwa sheria hii inatumiwa katika Shule za Umma za St. Louis, na

KWA KUWA, Baraza Kuu la Elimu, kupitia Azimio hili, linanua kuthibitisha kujitolea kwake ili kuwe mazingira ya usalama na ya kutia moyo kwa wanafunzi wote, bila kujali hali ya uhamiaji.

KWA HIYO, SASA, imeamuliwa na Baraza Kuu la Elimu la Jiji la St. Louis kama ifuatavyo:

1. Maombi yoyote kwa SLPS toka maafisa kwa kutaka kuteleza shughuli za sheria ya uhamiaji kwa shule lolote la SLPS yatajibiwa na Msimamizi/Mteule wake Msimamizi kwa kuhakikisha kumekuwa utiifu wa sheria. Shule hazitawaruhusu maafisa kama hao kukutana na wanafunzi shuleni bila kwanza wao wenyewe kuwasiliana na Ofisi ya Msimamizi na kutoa ombi lao na nyaraka zao ili kuchunguzwa.
2. Wafanyakazi wa SLPS watahughulikia wanafunzi wote na kutoa ulinzi sawa sawa kwao kama ilivyo katika sheria ya kutopendelea rangi, kabila, hali ya uhamiaji au asili ya mtu kitaifa.

IMEAMULIWA LEO _____ siku ya _____, 2025.

BARAZA KUU LA ELIMU LA JIJI
LA ST. LOUIS

Kwa: _____
Kiongozi

Thibitisha: _____
Katibu wa Baraza

4926-9154-2548, v. 2